

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA



## TAARIFA KWA UMMA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida kwa kushirikiana na Taasisi ya MO Foundation pamoja na MEDWELL Cheritable health Centre inayomilikiwa na Shirika lisilo la kiserikali (NGO) ya MEDWELL, **watatoa huduma ya kambi ya macho katika Hospitali ya Manispaa ya Singida kuanzia tarehe 2 Novemba 2023 hadi tarehe 4 Novemba 2023**

Huduma zifuatazo zitatolewa bila malipo:

- Kupima na uchunguzi wa macho
- Dawa za macho
- Miwani ya kusomea
- Huduma ya chakula kwa wagonjwa wote watakaolazwa kwa ajili ya upasuaji wa jicho

Wananchi wote mnaosumbuliwa na matatizo ya macho, mnajulishwa kufika Hospitali ya Manispaa ya Singida kwa tarehe zilizotajwa hapo juu ili kuweza kupata huduma hii adhimu. Usomapo tangazo hili mjulishe na mwingine

Imetolewa na:

**Kitengo cha mawasiliano serikalini**

**MANISPAA YA SINGIDA**

**31 Oktoba, 2023**